

TANZANIA / JUDGMENT

benjamin eliot makafu vs quality group ltd 2021 tzhcld 55 10 machi 2021

COURT
TANZLIIDECIDED
1 January 2021

Source: media.tanzlii.org · Research copy typeset by Esheria. Not court-issued or certified.

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA YA TANZANIA MAHAKAMA KUU
DIVISHENI YA KAZI KANDAYA DARES SALAAM MAOMBI YA MAREJEO NA. 434 OF 2019 BAINA
YA BENJAMIN ELIOT MAKAFU..... MLALAMIKAJI DHIDI YA QUALITY GROUP
LIMITED..... MLALAMIKIWA UAMUZI Tarehe ya mwisho ya Amri: 04/03/2021 Tarehe
ya Uamuzi: 10/03/2021 Z.G.Muruke, J. Benjamin Eliot Makafu aliajiriwa na mjibu maombi tarehe
17 Julai, 2017 kwa mkataba wa mwaka mmoja kama afisa tabibu (Medical officer) tarehe 03
Januari, 2018 mjibu maombi alisitisha ajira ya mleta maombi kwa sababu ya kufungwa kwa kazi
zilizokuwa zikiendeiea Mbagala kituo cha kazi cha mleta maombi. Mleta maombi alifuatilia haki
zake bila mafanikio hali iliyosababisha kupitwa na muda wa kufungua shauri, Alipeleka ombi la
kuongezewa muda (Tume) (CMA) ambako alikataliwa. Hakuridhika, hivyo kufungua marejeo
haya akiomba kutengua uamuzi wa Tume na kuona kwamba alikuwa ametoa sababu za kutosha,
na aruhusiwe kufungua mgogoro nje ya muda. i Mjibu maombi hakujibu hoja pamoja na wito
mara kadha kuwa ni pamoja na wito uliotolewa kwenye gazeti la Mwananchi la tarehe 31 Oktoba,
2019 ukurasa wa 37. Hata hivyo mjibu maombi hakutokea Mahakamani, na wala hakujibu hoja za
mleta maombi. Baada ya kujiridhisha, Mahakama ikaelekeza kesi iendelee upande mmoja tarehe
04 Novemba, 2020. Kwa kumuamuru mleta maombi kuleta majumwisho yake kabla ya tarehe 18
Novemba, 2020, na kesi kutajwa tarehe 30 Novemba, 2020. Tarehe tajwa, mleta maombi hakufika,
kesi ikapangwa kutajwa tarehe 04 Machi, 2021 ambapo Ezekiel Mayunga Mwakilishi wa mleta
maombi alikuwepo na hatimaye tarehe ya hukumu kupangwa leo. Majumwisho ya Wakii
yalijikita kwenye msingi wa haki ya kusikilizwa. Na kwamba mleta maombi alikosewa haki yake
ya msingi kwa kutosikilizwa. Hivyo aliiomba Mahakama, kufuta Uamuzi wa Tume na kuamuru
mleta maombi aruhusiwe kufungua mgogoro wake nje ya muda. Jambo la kuangaliwa ni endapo
mleta maombi alitoa sababu za msingi na za kujitosheleza mbele ya tume kuweza kuongezewa
muda:- Katika mwenendo wa shauri Tume CMA wa tarehe 28 Februari, 2019 mleta maombi
alieleza kuwa sababu ya kuchelewa kuleta maombi ilikuwa "ni yeye kufuatitia stahiki zake. Kwa
mjibu maombi kwa kumwandikia barua biia mafanikio," Hivyo ndiyo sababu pekee iliyoelezwa
na mleta maombi. Kumbukumbu zinaonyesha kuwa ajira ya mleta maombi ilisitishwa tarehe 03
Januari, 2018 na alifungua mgogoro tarehe 25 Septemba, 2018, ikiwa ni muda wa miezi 9. 2 Muda
wa miezi tisa, hauna maelezo yoyote toka kwa mleta maombi. Amesame alikuwa anafuatilia kwa
mjibu maombi kwa kuandika barua, lakini barua alizoandika hazijaambatanishwa kwenye ombi

stahiki. Sio tu barua bali mleta maombi alitakiwa kutoa mlolongo wa matukio wa kila siku kwa muda wa miezi tisa alichokuwa akifuatilia kwa mjubi maombi. Kutokuwepo kwa vielelezo barua alizoandika, na kukosekana kwa malezo ya kila siku iliyopita hadi kufikia meizi tisa ndiyo afungue ombi tume, ni tatizo. Tume au Mahakama haikubali maneno matupu bila uthibitisho. Kwa jinsi hiyo basi, Tume ilikuwa sahihi kukataa ombi la Benjamin Eliot Makafu. Hivyo basi Mahakama hii haioni sababu ya kutofautiana na Uamuzi wa Tume. Ombi hili limetupiliwa mbali, kwa kukosekana mashiko ya kisheria. . Z.G.Muruke JAJI 10/03/2021 Hukumu imesomwa leo mbele ya Ezekiel Mayunga, Wakili wa mleta maombi. Z.G.Muruke JAJI 10/03/2021 3

Source & reproduction note

Judgment wording, source notices and original paragraph numbers are retained. Esheria supplies the layout and this PDF's page numbers; these are not the source pagination. This is a research copy, not an official or certified court document. Check quotations, citations and publication restrictions against the original source before relying on it.

ORIGINAL SOURCE https://media.tanzlii.org/media/judgment/154804/source_file/benjamin-eliot-makafu-vs-quality-group-ltd-2021-tzhcld-55-10-machi-2021.pdf

CASE PAGE <https://chat.esheria.ai/case-law/tanzania/Extensionoftime-tanzlii-2021--6a3ea52a3b1caa9129823104>

Prepared on 26 October 2026 · Esheria